# TAARIFA YA PROGRAMU YA MAGEUZI YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA (PFMRP) MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA PFMRP-IV NA V KUANZIA MWAKA 2015/2016 HADI 2021/2022….

## 1.0 UTANGULIZI

Mradi wa Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) Zanzibar katika awamu ya tano ilikuwa katika lengo Namba 7 katika mpango mkakati wa PFMRP V. Lengo hili la kimkakati liliunganishwa na Mchakato wa Maendeleo ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na Maono 2020 na Mkakati wa pili wa Zanzibar wa Kukuza na Kupunguza Umasikini (MKUZA III - 2015-2020) ambayo inatambua mahitaji ya kutoa mapato bora ya ndani.

Lengo la kimkakati pia liliambatana na mfumo wa Matumizi ya Umma na Uwajibikaji wa Fedha wa Zanzibar (PEFA) 2010.

Lengo la Mradi ni kuimarisha usimamizi wa Fedha za Umma. Programu ya PFMRP inafadhiliwa kupitia "basket fund" kutoka kwa washirika wa maendeleo ambao ni Norway, DFID na Denmark. Hivyo Programu hii inahakikisha mapato na matumizi yanasimamiwa na kudhibitiwa kwa ufanisi mkubwa katika taasisi za Serikali na kuratibiwa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

Taasisi zinazonufaika na programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) kwa Zanzibar ni hizi zifuatazo: -

a) Baraza la Wawakilishi Zanzibar;
b) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
c) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali;
d) Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango;
e) Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali (ZPPDA);
f) Tume ya Mipango,
g) Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA); na
h) Wakala wa Serikali Mtandao (E-EGAZ).

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA –ZANZIBAR**

Mradi wa PFMRP umesaidia katika maeneo mengi ikiwa pamoja na kuanzishwa kwa mifumo inayoendelea kutumika katika taasisi mbali mbali. Pamoja na mambo mengine, PFMRP imeweza kufanikisha upatikanaji wa mambo yafuatayo:-

a) Uanzishwaji wa mfumo wa rejista ya mali na usimamizi wa mali za Umma (PIM), faida za mfumo huu ni kuiwezesha serikali kujua idadi ya mali zake ambazo inazimiliki, kujua hali halisi ilivyo(ukongwe/upya), kujua tarehe ununuzi, eneo ilipo, kushuka kwa thamani (depreciation) na thamani ya sasa ya kila mali, usahihi wa mali zilipo pamoja na mali zinazoondolewa. Mfumo wa rejista unasaidia kujua thamani ya mali za taasisi katika ufungaji wa hesabu za kila mwaka, pia kuwepo uwazi katika kuzijua mali za Serikali na kujua inamilikiwa na nani na kiasi gani.

b) Uanzishwaji wa ZAN-MALIPO umechangia kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

c) Utengenezaji wa Mfumo wa Bajeti na Matumizi (BAMAS). Mfumo huu utakapoanza kutumia utaleta tija na kusaidia kupunguza gharama za kila mwaka za kulipia leseni na "service levy" kwa "consultancy firm", kupatikana ufanisi kwa kutatua matatizo ya mfumo kwa wakati kwa kutumia wataalamu wa ndani, kusomana (system integration) kwa mifumo ya kibenki, mfumo wa utumishi (HRMS), Zan Malipo na kadhalika, Mfumo wa BAMAS utapunguza "manual transactions" katika mapato na matumizi, utakuwa na urahisi wa utumiaji wa mfumo (user friendly).

d) Uanzishwaji wa mfumo wa ukaguzi (GARI-ITS), faida za mfumo huu ni kurahisisha ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ndani na nje, kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa kazi za Serikali, kusaidia uhifadhi wa kumbukumbu za kazi za ukaguzi, na kurahisisha utafutaji wa taarifa za ukaguzi.

e) Uanzishwaji wa "Human Resource Management Information System" (HRMIS and Payroll), tayari taasisi tano zimeanza kuingizia taarifa (demo)- ambazo ni Wizara ya biashara, Kamisheni ya utalii, Halmashauri ya kaskazini A, Magharibi A, tume ya

kurekebisha sharia. Faida za mfumo utakapokamilika taasisi zote zitaingiza taarifa zake wenyewe, na pia itasaidia upatikanaji wa taarifa za watumishi kwa haraka na usahihi.

f) Uandaaji wa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango,

g) Uandaaji wa Mpango Mkakati wa PFM kwa upande wa Zanzibar,

h) Mpango Mkakati wa "Digital" kwa Zanzibar,

i) Ununuzi wa Vifaa wa TEHAMA zikiwemo "servers" za mifumo iliyotajwa hapo juu.

j) Kuwajengea uwezo taasisi zote zinazonufaika na programu ya PFMRP ambazo ni ZPPDA, OCAG, IAG, OTR, idara ya Bajeti, Baraza la Wawakilishi, idara ya Mhasibu Mkuu, Idara ya Fedha za nje, Tume ya Mipango, Idara ya Sera za Fedha na Kodi katika fani tofauti, na wadau wote wa mifumo iliyotajwa hapo juu.

k) Uimarishaji wa Usimamizi na udhibiti: Ukaguzi wa ndani na Ukaguzi wa nje wa Serikali Umeimarika. Kwa kuzingatia na dhamana ya ukaguzi wa fedha kwa kuwajengea uwezo watendaji wa taasisi husika.

l) Uanzishwaji wa utumiaji wa bajeti inayotumia program (PBB) kwa Serikali za Mitaa hadi ngazi za madiwani. Aidha, mafunzo katika uandaaji na uchambuzi wa Bajeti yamesaidia kuimarisha ufanisi na utendaji wa majukumu.

m) Kuimarisha mfumo wa mishahara ambapo risiti zinapatikana kupitia mitandao kwa kupunguza msongamano. Hatua hii imeleta ufanisi katika kazi na utendaji.

n) Watendaji wa kada mbalimbali kwa taasisi tofauti wamejengewa uwezo na kuongezewa ujuzi wa utendaji kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika utumiaji wa mifumo, ikiwemo kada za ununuzi na uhasibu.

o) Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa wafanyakazi zaidi ya 500 wa taasisi zote zinazonufaika na PFMRP katika fani mbali mbali ikiwemo utayarishaji wa mpango mkakati, Mafunzo kwa wafanyakazi juu ya mapato yasiyo ya kodi, Uhamasishaji wa

kutumia PBB kwa maofisa wa Serikali, Kujenga Uwezo kwa Kitengo cha Usimamizi wa Madeni ya Umma, mafunzo kuhusu taarifa za fedha kwa Wahasibu Wakuu, mafunzo ya Tehama kwa kitengo cha IFMS, mafunzo kwa wahasibu wakuu juu ya ufahamu wa "IPSAS and Accrual basis", uchambuzi wa fedha ambazo zinahitajika katika ukusanyaji wa mapato.

p) Kuanzishwa na kuanza kutumika kwa mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa shughuli za ZRA, ambapo hivi sasa shughuli za matumizi (expenditure) na shughuli za Mchakato wa Zabuni za ZRA zinafanyika kwa kutumia mfumo huu.

q) Ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kielektroniki kwa matumizi ya ofisi (electronic equipment) kwa ZRA zikiwemo kompyuta za Mezani na Kompyuta mpakato ambazo zimepunguza changamoto ya upungufu wa vitendea kazi pamoja na kurahisisha utendaji na kuleta ufanisi ambapo wafanyakazi wengi wanaweza kufanyakazi kwa wakati mmoja.

r) ZRA hivi sasa inafanya uchunguzi wa kodi kwa kutumia maabara ya kuchunguza taarifa za kikodi zilizotunzwa au kuhifadhiwa katika mifumo ya kielektroniki (Forensic lab) na kugundua kodi ambayo ilikuwa imefichwa katika mifumo ya wafanyanyabiashara.

***s)*** Kujengwa kwa kituo Kikuu cha kuhifadhia taarifa (ZRB Data Centre) ambapo taarifa zote za kikazi zipo salama katika mfumo huo.

***t)*** Kutengenezwa kwa Mpango Mkakati wa Nne wa ZRA ambao unaonesha muelekeo wa ZRA hadi kufikia mwaka 2024/2025.

## 2. 0 HITIMISHO KWA MAFANIKIO YA HADI 2021/2022

Utekelezaji wa miradi hii chini ya ufadhili wa Wadau wa Maendeleo, na jitihada mbali mbali za ndani zilizochukuliwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na zimeimarisha utendaji kazi kwa kupata vifaa, mifumo ya kielektroniki na ujuzi kwa wafanyakazi na hatimaye kuweza kuongeza mapato ya Serikali na kuwezesha kuimarisha usimamizi mzuri wa Fedha za Umma.

## 3. 0 PROGRAMU YA MABORESHO YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA AWAMU YA SITA (PFMRP VI) –ZANZIBAR

**Mhesimiwa Mwenyekiti,** Lengo la Programu ni kuimarisha usimamizi wa Fedha za Umma. Mpango Mkakati wa PFMRP VI umeandaliwa kwa kulenga mageuzi kupitia malengo matano ya Kimkakati yaliyoainishwa kutokana na vipaumbele ambavyo vitapelekea kuimarika kwa uchumi na uimarishaji wa utoaji huduma kwa jamii.

Kwa upande wa Zanzibar, lengo la kimkakati wa PFMRP VI linaambatana na mfumo wa Matumizi ya Umma na Uwajibikaji wa Fedha wa Zanzibar (PEFA) 2018 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 ambayo inabainisha usimamizi wa fedha za umma kuwa ni kipaumbele kwa kuzingatia uhamasishaji wa mapato ya ndani.

Mpango mkakati wa PFMRP VI ulitayarishwa na wataalamu wa ndani kutoka Taasisi zote husika na PFMRP. Utekelezaji wa PFMRP VI ni wa miaka mitano kuanzia tarehe 1 Julai 2022 hadi tarehe 30 Juni 2027. Jumla ya Fedha zote zilizopangwa kwa kipindi cha miaka mitano ni TZS 158 bilioni, ambapo kwa Zanzibar ni TZS 20 bilioni.

Mpango mkakati huo unalenga katika vipaumbele vifuatavyo: -

a) “Domestic revenue collection and external resources management improved”,
b) “Budget management”,
c) “Financial management and reporting”,
d) “Procurement and asset management”, and
e) “Audit and Oversight functions2.

Taasisi zinazonufaika kupitia Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP VI) kwa upande wa Zanzibar ni kama zifuatazo:

a) Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA);
b) Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA);
c) Ofisi ya Baraza la Wawakilishi (HoR);
d) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (OCAG);

e) Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango (PO-FP), Zanzibar;
f) Tume ya Mipango, Zanzibar (ZPC);
g) Ofisi ya Msimamizi wa Hazina (OTR);
h) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (OIAG);na
i) Wakala wa Serikali Mtandao (e-GAZ).

**MATUMIZI YA FEDHA ZA MRADI.**

Kwa mwaka wa fedha wa fedha 2022/2023 Programu hiyo ina bajeti ya jumla ya TZS 3.7 Bilioni, Utekelezaji wa PFMRP VI ni wa miaka mitano kuanzia tarehe 1 Julai 2022 hadi tarehe 30 Juni 2027.